Climate Information for Grains

EASTERN AFRICA GRAIN COUNCIL






# JUKWAA LA MAWASILINO JUU YA USIMAMIZI WA NAFAKA BAADA YA MAVUNO

## MWONGOZO WA MAFUNZO

www.ci4g.net






Shukrani ..... 1

Historia ..... 2

Utangulizi katika Jukwaa la CI4G ..... 3

Moduli 1: Utangulizi katika jukwaa la CI4G ..... 3

Yaliyomo katika mfumo wa CI4G ..... 3

Moduli 2: Tovuti ya CI4G ..... 3

Moduli 3: Ushauri wa Mazao ..... 6

Moduli 4: Jukwaa la SMS la CI4G ..... 7

## SHUKRANI

Baraza La Nafaka La Afrika Mashariki (EAGC) linatambua mchango wa mtandao wa hali ya hewa na masuala ya stadi za maendeleo wa Climate & Development Knowledge Network(CDKN), kupitia mradi wake wa kupunguza hasara baada ya mavuno na uongezaji uzalishaji, unaoepuka madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa nchini Kenya na Uganda.Hata hivyo matokeo hayo ni pamoja na mchango wa jukwaa la hali ya hewa kwa wadau wa uzalishaji mazao ya nafaka lijulikanalo kama (CI4G).

Hata hivyo EAGC inatambua pia ushirikiano na mchango wa kitaalam kutoka kituo cha utabiri wa hali ya hewa cha IGAD na ICPAC, mamlaka ya Udhibiti wa Majanga nchini Kenya NDMA, Wizara ya Kilimo na Sekta ya Wanyama na Uvuvi nchini Uganda (MAIFF).

Ukuaji wa majukwaa ya uzalishaji wa nafaka umetokana na mchango wa wadau wa ongezeko la mnyonyoro wa thamani, ambapo utafiti wa ongezeko la thamani ulifanywa kuanzia ngazi ya awali ya mradi, huku kukiwa na uhitaji mkubwa wa taarifa za hali ya hewa, kama vile jotoridi, kiwango cha mvuke,unyevunyevu na kujua kasi na ulekeo wa upepo karibu na maeneo ya uzalishaji.

Hata hivyo maendeleo yaliyofikiwa ni kutokana na jitihada za CI4G, huku EAGC ikitoa shukrani za pekee, kwa wadau wa ongezeko la thamani ya mazao.

EAGC inawashukuru pia wadau wote, katika ongezeko la thamani la nafaka ambao,waliweza kutoa mrejesho wa namna walivyotumia ushauri wa watalaamu wa kilimo kupitia majukwaa ya EAGC CI4G, kwa lengo la kujua muda sahihi wa kupanda, kuvuna na ukaushaji wa mazao ili yasipungue thamani.Lakini pia kujenga mazingira ya kuandaa fursa za soko kwa kile wanacho kizalisha.

Funded by

Kazi hii ilikamilishwa kwa msaada wa wizara ya mambo ya nje ya Uholanzi na umoja wa watafiti wa maendeleo kimataifa (IDRC), Na Canada kama moja ya mpango elimu juu ya tabia ya nchi. Maoni yaliyotolewa humu hayana uhusiano wowote na wizara ya nje Uholanzi au IDRC wala bodi yake ya uongozi au vyombo vinavyoisimamia CDKN

Hatimiliki © 2020, Climate and Development Knowledge Network. Haki zote zimehadhiwa.

## UTANGULIZI

Kitovu cha taarifa za nafaka yaani CI4G portal ni jukwaa shirikishi linalo wawezesha wadau wa ongezeko la thamani kupata taarifa za hali ya hewa na ushauri wa watalaam wa mazao ya kilimo, namna ya usimamizi wa kuepuka hasara baada ya mavuno,soko na ushauri wa wataalamu wa kilimo pia.Taarifa za hali ya hewa kwa mazao ya nafaka na ushauri wa mazao mengine kama vile mahindi,maharage,ngano na njegele zinatolea katika vituo hivyo vya CI4G,chini ya uratibu wa vituo vya biashara ya nafaka, kinachoitwa EAGC Grain Trade Business Hubs (GHUBs). GHUBs, ndipo kitovu cha makundi ya wakulima wadogo wadogo kinachotoa huduma za pembejeo kama vile mbegu,mbolea mafunzo ya matumizi ya mashine za kilimo, taarifa za hali ya hewa,na uuzaji wa mazao yao kwa pamoja kupitia mfumo wa soko ujulikanao kama EAGC's GSOKO. Wadhibiti ongezeko la thamani la nafaka, hupata ushauri wa wataalam wa kilimo katika vituo yaani (GHUBs),na pia wamekuwa wakifuatilia taarifa za hali ya hewa, zinazotolewa na ICPAC, ambazo hupatikana ndani ya eneo la upana wa maili tisa,na taarifa hizo hubadilishwa kila siku kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa ya kila siku.

Watalaam wa uzalishaji wa mazao na usimamizi wa udongo ndiyo watumiaji wa maudhui ya tovuti ya Ci4g.net, na pia maudhui hayo yanasimamiwa na maofisa mradi wa EAGC na wadau wa mradi kwa ujumla.

Jukwaa hili pia hutoa huduma ya ujumbe mfupi wa maandishi SMS, ambapo kupitia kifaa maalumu, wadau wote katika mpango huu wanaweza kupata ujumbe wa kimakundi kwa mara moja.

Muongozo huu utatumika kutoa mafunzo kwa wadau wa ongezeko la thamani la mazao ama nafaka chini ya CI4G ili kuwawezesha kuwa na maamuzi stahiki katika kuamua ni wakati gani wa kupanda au kuvuna,ukaushaji wa mazao,utunzaji,ikiwa ni moja ya sababu ambazo huchangia kupunguza bei na kusababisha hasara itokanayo na uvunaji.Lakini wakati huo,CI4G itawawezesha kutafuta fursa ya soko la kile wanacho kizalisha.






*Figure 1: CI4G functionality*

# UTANGULIZI WA JUKWAA LA CI4G

## Moduli 1: Utambulisho wa jukwaa la CI4G

Kuna vipengele vitatu vinavyo unda jukwaa la CI4G ambavyo ni kama vifuatavyo:-
Kipengele cha kwanza ni takwimu zinazo ingia,yaani zinazo zalishwa ama kupatikana hapo kituoni, mbili ni kipengele cha uchakataji wa takwimu ama taarifa. Katika hatua hii,ndipo taarifa zinapangwa na kuwekwa katika mfumo rahisi zaidi,ili ziweze kueleweka kwa urahisi na watumiaji,na kisha zinahifadhiwa.Hatua ya tatu na ya mwisho ni zile taarifa zilizoainishwa tayari kwa matumizi (synthesized information),hizi ndizo hutumwa katika chaneli mbali mbali kupitia ujumbe mfupi wa maneno yaani SMS, ama kupitia tovuti ya CI4G kama hatua ya awali ya kushirikisha watumiaji.




### Malengo ya Moduli

Moduli hii inalenga kuwabainisha watumiaji wa CI4G, ili kuwawezesha kuwa na uelewa mpana kuhusiana na jukwaa, na namna ya upataji taarifa.Hata hivyo pia watawezeshwa kujua namna ya kuzichakata taarifa hizo, na kupata ulewa kamili wa mfumo wa uzalishaji wa taarifa kupitia program hii ya CI4G.

**maswali ya Kujikumbusha:**

1. Namna gani CI4G ilianzishwa?
2. Ni kundi gani la awali lililolengwa na mfumo huu wa CI4G?

# MAENEO MUHIMU YA MFUMO WA CI4G

## MODULI 2: TOVUTI YA CI4G

### Utangulizi wa Moduli

Watumiaji kupitia moduli hii watafundishwa namna ya kurambaza ama matumizi sahihi ya tovuti hii ya CI4G, ambayo ni hatua ya awali katika kuwasaidia watumiaji kupata taarifa za utabiri wa hali ya hewa na ushauri.

### Malengo ya Moduli


Kujenga uwezo kwa watumiaji juu ya namna ya upataji taarifa katika tovuti ya CI4G.

**Maudhui ya Moduli**

- Kubainisha /ama uchaguzi wa eneo
- Ufafanuzi/Tafsiri ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.

## Tovuti

**a. Namna ya kuingia bonyeza ci4g.net**





**b. Kupokea taarifa za utabiri wa hali ya hewa**


i Chagua bidhaa

ii Chagua hatua ya mazao
- Maandalizi ya ardhi
- Upandaji na ukuaji wa mboga mboga.
- Palizi
- Mazao kubeba hadi kukomaa
- Mavuno na baada ya mavuno

iii Chagua eneo au kitovu
- Ushirika wa Challa Njukini
- Marungu Kupojo Coop
- Jumuiya ya wazalisha nafaka ya Tharaka
- Makandi Mwangaza CBO
- Kabisaga CBO
- Naima CBO
- Ushirika wa wakulima wa Mathangauta
- Ushirika wa Msinduka
- Ushirika wa Wakulima wa Kitise
- Katheka CBO
- Indatwa Cooperative
- Ushirika wa Coopamuja
- Ushirika wa Gwiza
- Katerera
- Kitovu cha Katine

iv Bofya/bonyeza kitufe cha utabiri
- Kiwango cha jotoridi katika kipimo cha sentigrade na kiwango cha mvua katika milimita.
- Kipimo cha joto katika kiwango cha juu na cha chini.
- Uelekeo wa upepo na kasi yake.
- Kiwango cha unyevu nyevu.
- Utabiri wa kila siku wa hali ya hewa katika kila kituo, kuangalia kiwango cha joto na uwezekano wa mvua.
- Tahadhari za hali ya hewa,ikiwemo utabiri wa majira.



C4G

HOME ADVISORIES SMART CLIMATE DIRECTORY MAP HISTORICAL CONTACT


AGRO - ADVISORIES

HOME / AGRO ADVISORIES

Showing **1-20** of **105** items.

| # | Location | Ward | Crop | Crop Stage | Advisory |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tharaka Cereal Growers Coop. Society | Tharaka Nithi | BEANS | Land preparation for planting | Prepare land with minimal soil disturbance e.g using rippers and Plant certified and drought tolerant seeds since low rainfall is expected |
| 2 | Challa Njukini coop | Taita Taveta | MAIZE | Harvesting | The farmers need to start aggregating good quality grains engage traders on structured negotiations for trading in grains. |
| 3 | Challa Njukini coop | Taita Taveta | MAIZE | Harvesting | The farmers should repair, clean and fumigate stores and aggregation centres/warehouses in preparation for storing grains. |
| 4 | Marungu Kupojo Coop | Taita Taveta | MAIZE | Harvesting | The farmers should repair, clean and fumigate stores and aggregation centres/warehouses in preparation for storing grains. |
| 5 | Tharaka Cereal Growers Coop. Society | Tharaka Nithi | MAIZE | Harvesting | The farmers should repair, clean and fumigate stores and aggregation centres/warehouses in preparation for storing grains. |
| 6 | Makandi Mwangaza CBO | Meru | MAIZE | Harvesting | The farmers should repair, clean and fumigate stores and aggregation centres/warehouses in preparation for storing grains. |
| 7 | Kabisaga CBO | Nandi | MAIZE | Harvesting | The farmers should repair, clean and fumigate stores and aggregation centres/warehouses in preparation for storing grains. |

**c. Pia unaweza kutumia ramani inayooonyesha vituo mbalimbali.**



d. **Pia unaweza kupata historia ya taarifa za mvua kutoka katika vituo 24 nchini Kenya.**

C4G CLIMATE INFORMATION FOR THE GRAIN SECTOR

HOME ADVISORIES SMART CLIMATE DIRECTORY MAP

Showing **1-20** of **7,944** items.

| # | Location | Year | Month | Precipitation |
|---|---|---|---|---|
| 1 | LODWAR | 1981 | Jan | 0 |
| 2 | LODWAR | 1981 | Feb | 0 |
| 3 | LODWAR | 1981 | Mar | 43.2 |
| 4 | LODWAR | 1981 | Apr | 13.6 |
| 5 | LODWAR | 1981 | May | 1.7 |
| 6 | LODWAR | 1981 | Jun | 0 |
| 7 | LODWAR | 1981 | Jul | 0 |

**Moduli 2: Maswali ya Kujikumbusha**

1. Namna gani ushauri unatolewa?
2. Ni kwa namna gani utabiri wa hali ya hewa unahitajika?
3. Je ni kwa namna gani taarifa za watabiri wa hali ya hewa zinatafsiriwa na watumiaji?

## MODULI 3: USHAURI WA MAZAO

### Utangulizi wa Moduli

Ushauri wa mazao una patikana kutokana na uchambuzi yakinifu wa data uliofanywa na EAGC, ambao ndiyo waratibu wa wawakilishi kutoka eneo la mradi. Hata hivyo wanapata taarifa kutoka kwa mashirika mengine ama kituo cha utabiri wa hali ya hewa wa kituo cha (ICPAC). Ushauri huu huwafikia wadau katika maeneo yao,na kuwasaidia kupata ongezeko la thamani ya kile wanacho kizalisha katika maeneo yao. Ushauri wa mazao unaotolewa unalenga ufanisi katika matumizi sahihi ya udogo,uhifadhi wa mazao,usafirishaji na suala la masoko. Hata hivyo ushauri wa mnyonyoro wa thamani unaanzia shambani hadi kumfikia mtu wa mwisho.

### Malengo ya Moduli

Kutoa uelewa wa hatua za upatikanaji wa ushauri wa mabadiliko ya tabia nchi.

Nini cha kujifunza kutoka katika moduli hii:

1. Jinsi gani ushauri hutolewa
2. Namna gani ushauri unavyochapishwa katika tovuti ya CI4G
3. Jinsi gani jumbe zinasambazwa kwa kutumia teknolojia ya Bulk

## MFANO WA USHAURI

### KENYA

Katika mwezi Oktoba /Novemba 2020 taarifa zina onyesha kuwa, eneo la magharibi mwa Kenya lina uwezekano wa kupata kiwango cha mvua zaidi ya matarajio wakati eneo la Mashariki linatarajiwa kupata wastani wa chini wa kiwango cha mvua. Hata hivyo mwezi Oktoba unatarajiwa kushuhudia mwanzo wa vipindi vya mvua katika baadhi ya maeneo ya nchi. Maeneo ya magharibi mwa Kenya mvua, zitaendelea kuanzia mwezi Septemba 2020, japo kuwa maeneo mengine ya nchi mvua zitaanza juma la tatu la mwezi Oktoba hadi juma la kwanza la mwezi Novemba 2020.

Katika eneo la uwanda wa juu Magharibi mwa bonde la ufa,bonde la ziwa Victoria, bonde la kati la ufa, pamoja na Kaskazini na Kaskazini Magharibi mwa Kenya,yana tarajiwa kuwa na vipindi vya mvua za wastani. Maeneo mengine ya nchi yana tarajiwa kuwa na mvua za chini ya kiwango.

### UWANDA WA MASHARIKI YA JUU, THARAKA NITHI, MERU, EMBU

Mazao yanayolimwa katika eneo hili la uwanda wa juu wa Mashariki ni mahindi,njegere,kunde na mtama. kwa sasa wakulima walio wengi wapo katika baadhi ya hatua za maandalizi ya ardhi, upandaji wa mbegu na ununuzi wa mbolea.

- Kufuatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa zinazoonyesha uwezekano wa ukanda wa Mashariki kuwa na kiwango kidogo cha mvua,wakulima wameshauriwa kulima mazao yanayo stahimili ukame na ya muda mfupi.
- Kuhusiana na suala la matumizi ya mbolea, wakulima wameshauriwa kuwa waangalifu, kwani wanaweza kuhatarisha mbegu ama kuifanya ioze kutokana na ukosefu wa mvua wanapaswa kuzingatia maelezo ya utabiri wa hali ya hewa na ushauri kutoka kwa watalaam wa ardhi ama wizara ya kilimo.

### KANDA YA MAGHARIBI

Mazao yanayolimwa ukanda huu wa Magharibi ni mahindi, maharage na mtama. Na kipindi hiki walio wengi wanavuna, wanakausha mazao yao na kuyauza.


**Ushauri wa Mazao**


- Maeneo ya ukanda huu, yanatarajiwa kuwa na mvua zaidi ya wastani,kutokana na hali hiyo wakulima wana shauriwa kuacha kuvuna na kuanika mazao yao siku za mvua.
- Ili kuhifadhi ubora wa mazao,inashauriwa kuanika kwa kutumia maturubai na kuyahifadhi mazao hayo ndani ya mifuko ama kuwa na vifaa vingine vya kukaushia mazao pia.
- Utambuzi wa vyama vya ushirika, vilivyo karibu na wakulima kwaajili ya soko la mazao yao.
- Maandalizi ya mifuko ya kuvunia, ununuzi wa maturubai,ukaushaji na uhifadhi wa mahindi na maharage.


## MODULI YA 4: JUKWAA LA UJUMBE LA CI4G

## Utangulizi

Watumiaji wa huduma ya CI4G watapata nafasi ya kuelekezwa namna gani platform ya kutuma jumbe inavyotumika kutuma taarifa kwa wakulima . ujumbe hupokelewa kwa kutumia mfumo wa Gateway ambao hufanya kazi kushirikiana na program ya bulk. Mfumo huu wa huwafikia kwa kutumia EAGC's Gateway. Wakulima kutoka katika kila kituo hupokea ujumbe mfupi wa hali ya hewa katika maeneo yao.




RATIN data in local currency
Kenya
Uganda
Tanzania
Rwanda
Burundi
South Sudan
Malawi
DRC
Select Language
RATIN
ADVERTISE YOUR BUSINESS HERE
RATIN data will be limited to authorized subscribers from 15th August 2018.
To subscribe, please get in touch with EAGC on ratin@eagc.org
Home
About
Markets
Crossborder Trade
Warehouses
News & Bulletins
Resources
Contact Us
Currency & Packaging
Login
Major East African Markets Prices for the Last 7 days
Major East African Markets Prices for Mixed Beans
1200
1000
800
600
News
EALA member warns region against overspending
EALA member warns region against overspending in imports of fodstuff
Kenyans anticipate Cabinet's decision over lifting
Kenyans anticipate Cabinet's decision over lifting ban on GMOs
Radical proposals to save Kenya's ailing agricultu
Kenya: Radical proposals to save Kenya's ailing agriculture
Weather problems having little impact on market
Weather problems having little impact on market
Rwanda-Hungary Business Forum seeks to showcase

Kwa taarifa zaidi kuhusu CI4G wasiliana na:

## BARAZA LA NAFAKA LA AFRIKA MASHARIKI


**Regional Head Office & Kenya Country Office**
Lavington, Mbaazi Avenue, Off Kingara Road
P.O. Box 218, 00606 Nairobi, Kenya
Cell: +254 733 444035, +254 710 607313
Email: grains@eagc.org

**Tanzania Country Office**
Mikocheni B, Ruvu street, House no 2,
Dar es salaam
P.O. Box 33619 ,Dar Es Salaam
grains_tz@eagc.org

**South Sudan**
Juba Raha Camp
Next to JIT Super market
P.O Box 373 Juba -South Sudan
Tel:+211 925 787 123

**Rwanda Country Office**
House No.16 Kabaya Village, Rwimbogo Cell
Nyarugunga Sector, Kicukiro District
P.O. Box 4497 Kigali
Tel: +250 788 313 998/ +250 788 315 138

**Malawi Country Office**
Room 13, Anamwino House
P.O. Box 30395 Capital City,
Lilongwe 3
Tel: +265 999 975 994/999 975 899

**Zambia Country Office**
C/o Grain Traders Association of Zambia
Katanga Road
P.O. Box 34863 Industrial Area,
Lusaka, Zambia

**DR Congo**
P.O Box 308 Goma
Tel:+243 994 908 489

**Burundi - Bujumbura**
Tel +257 714 80983